**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

# ALIYOELEKEZA DKT. RWEZIMULA KUHUSU KUIMARISHA UMAHIRI WA WANAFUNZI WA UFUNDI STADI

TAREHE 4 MEI, 2023



- **Kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya vyuo vya ufundi stadi na viwanda**
- **Kufanya marejeo ya mara kwa mara ya mitaala kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira**
- **Ameishauri VETA kushirikiana na wadau ili kusaidia wahitimu wa ufundi stadi kupata mikopo na misaada mingine ya kifedha ili kuwasaidia kujiajiri**

**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**



## Aliyoelekeza Dkt. Rwezimula kuhusu kuimarisha umahiri wa wanafunzi wa ufundi stadi

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Rwezimula, tarehe 4 Mei 2023 alifanya ziara katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na kuelekeza mambo kadhaa yanayoweza kuchangia katika kuongeza ubora wa mafunzo, hivyo umahiri wa wanafunzi wa ufundi stadi.

Akizungumza na Menejimenti ya VETA Makao Makuu, miongoni mwa mambo aliyoelekeza Dkt, Rwezimula ni kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya vyuo vya ufundi stadi na viwanda ambako vijana wanaweza kupata mafunzo mengi ya vitendo na kujifunza teknolojia za kisasa zaidi, sambamba na kuboresha karakana kwa kununua vifaa vya kisasa na kuona namna ya kutumia wabobevu wa ufundi kutoka mfumo usio rasmi kusaidia kwenye mafunzo ya vitendo.

Mambo mengine aliyoyaagiza, Dkt. Rwezimula ni pamoja na kufanya marejeo ya mara kwa mara ya mitaala ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira ili utoaji mafunzo uendane na mahitaji ya soko la ajira na shughuli za kiuchumi katika jamii mbalimbali na pamoja na kufanya ufuatiliaji wa wahitimu ili kutambua wanavyokubalika na wanavyofanya kazi kwenye soko la ajira.

"Tunapokwenda kwenye mabadiliko ya mitaala ya elimu nchini, ufundi stadi ni suala la msingi. Pia uchumi wa sasa uko kwenye ufundi zaidi. Kwa hiyo, ni muhimu kutambua na kuzingatia majukumu ya VETA katika kusaidia mwelekeo huu," alisema.

Kwa upande mwingine, Dkt. Rwezimula ameishauri VETA kushirikiana na wadau ili kusaidia wahitimu wa ufundi stadi kupata mikopo na misaada mingine ya kifedha ili kuwasaidia kujiajiri.



Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Ethel Kasembe, alieleza juhudi za Wizara katika kusaidia uboreshaji mafunzo kuwa ni pamoja na kuandaa maandiko ya kuomba fedha za kununua vifaa vya karakana kwa ajili ya mafunzo kwenye vyuo vya VETA nchini.



Akitoa taarifa ya maendeleo ya uendeshaji wa shughuli za VETA, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, licha ya kutaja mafanikio mbalimbali alitaja uhaba wa vifaa kwenye karakana za mafunzo, uhaba wa watumishi na ukomo mdogo wa bajeti ikilinganishwa na hali ya kukua na kupanuka kwa Mamlaka kuwa ni miongoni mwa changamoto.

Alitaja miongoni mwa mafanikio kuwa ni pamoja na kufanya tafiti kumi (10) za soko la ajira; kutoa...

mafunzo kwa wajasiliamali 708 kupitia programu ya INTEP katikamwaka 2022/2023; kuibua wabunifu 82 kutoka vyuo vya ufundi stadi na 573 kutoka mfumo usio rasmi walitambuliwa kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) katika kipindi cha mwaka 2019-2022 na kuboresha na kufanya marejeo ya mitaala 48 kati ya 89 ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika mwaka wa fedha 2022/2023 na umaliziaji wa vyuo 25 vya wilaya, pamoja na utengenezaji wa samani zake.

CPA Kasore alitaja mafanikio mengine kuwa ni kudahili wanafunzi 46,379 kwenye vyuo vya VETA katika kipindi cha nusu mwaka 2022/2023 na wanafunzi 243 wenye mahitaji maalum.



Hata hivyo, CPA Kasore alitaja changamoto zinazoikabili Mamlaka kuwa ni pamoja na ukomo wa bajeti kutotosheleza mahitaji ya shughuli za Mamlaka kwa ujumla; mahitaji ya vifaa na upungufu wa watumishi.

“Mathalani, mwaka 2022/2023 Mamlaka imetengewa bajeti ya Shilingi 54,000,000,000/= ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Shilingi 99,600,000,000/=. Mahitaji ya vifaa vyuo vyote vya VETA ikiwemo 65 vinavyojengwa yanakadiriwa kufikia TZS. 211,047,890,669.00. Pia tuna upungufu wa watumishi 1282,” alifafanua.

Alimuomba Naibu Katibu Mkuu kwa niaba ya Wizara kupokea maombi ya kuongezewa bajeti ya uendeshaji kutokana na kukua kwa Taasisi hususani kuongezeka kwa idadi ya vyuo ambapo kufikia 2024 VETA itakuwa na vyuo zaidi ya 140 ikilinganishwa na vyuo 51 vilivyopo sasa. Vilevile gharama za uendeshaji mafunzo zimekuwa zikipanda mwaka hadi mwaka.

Vilevile kusaidia upatikanaji wa vibali vya ajira kwa ajili ya watumishi walimu na wasio walimu ili kufanikisha kuanza kwa mafunzo katika vyuo vipya vinavyokamilika kujengwa na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya vifaa vya mafunzo (tools and equipment) kwa ajili ya vyuo vya zamani na vyuo vipya 33 ambavyo ujenzi unakamilishwa.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula alipotembelea Kiwanda cha Samani VETA Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula alipotembelea Karakana ya Mafunzo ya Uandaaji wa Chakula Chuo cha VETA Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula alipotembelea Karakana ya Mafunzo ya Ufundi Bomba Chuo cha VETA Dodoma.

Aliyoelekeza Dkt. Rwezimula kuhusu kuimarisha umahiri wa wanafunzi wa ufundi stadi

UK. 04



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula alipotembelea Karakana ya Mafunzo ya Uungaji Vyuma (Uchomeleaji) Chuo cha VETA Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula akikagua Ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Chamwino.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula akikagua Ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Chamwino.



Wananchi wa Kijiji cha Bwawani wakishiriki Ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Chamwino.

# UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA

VETA